



TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.

KKKT Dayosisi ya Meru inapenda kutangaza nafasi ya kazi kama ilivyoainishwa.

Nafasi: Katibu Mkuu wa Dayosisi.

1. Wajibu wa Katibu Mkuu wa Dayosisi

Wajibu wa Katibu Mkuu umeainishwa katika Katiba ya KKKT Dayosisi ya Meru kama ifuatavyo:-

- i. Atakuwa Mtendaji Mkuu wa kazi za Dayosisi
- ii. Atakuwa Msimamizi Mkuu wa mambo ya fedha.
- iii. Atahakikisha kuwepo utaratibu mzuri wa Ki-Utawala kwenye Majimbo, Sharika na Vituo vya Dayosisi.
- iv. Ataandaa agenda za Mkutano Mkuu, Halmashauri Kuu, Kamati ya Utendaji na Fedha na Kamati ya Maofisa akishirikiana na Mkuu wa Dayosisi (Askofu).
- v. Ataona kuwa miniti za Mkutano Mkuu, Halmashauri Kuu, Kamati ya Utendaji, Kamati ya Maofisa, Halmashauri nyingine zinaandikwa vizuri na kushughulikia utekelezaji wa mapatano ya vikao hivyo.
- vi. Atatunza ripoti zote, miniti zote na maandishi yote ya Dayosisi.
- vii. Atakusanya na kutunza takwimu (Statistics) zote za kazi za Dayosisi.
- viii. Atahudhuria mikutano ya Halmashauri na Kamati nyingine za Dayosisi akiwa Mjumbe mwenye sauti bila kura.
- ix. Atatunza muhuri Mkuu wa Dayosisi.
- x. Atakuwa mmojawapo wa wadhamini wa mali za Dayosisi.
- xi. Atatunza kazi nyingine yoyote atakayokabidhiwa na Askofu, Msaidizi wa Askofu ama Halmashauri Kuu ya Dayosisi.
- xii. Atashauriana na Wakuu wa Idara na Vituo kuhusu mambo ya Utendaji

2. Sifa za muombaji

- i. Awe Mkristo Mlutheri mwaminifu.
- ii. Awe na Elimu kuanzia ngazi ya Shahada katika Uongozi.
- iii. Awe na utaalamu wa matumizi ya computer na vifaa vingine vya mawasiliano.
- iv. Awe tayari kufanya kazi muda wa ziada bila malipo ya ziada.
- v. Awe tayari kusafiri mara kwa mara.
- vi. Mwenye utaalamu wa mambo ya fedha na uongozi watafikiriwa zaidi.
- vii. Awe na Leseni hai ya Udereva.
- viii. Awe tayari kuanza kazi mara moja.

Barua ya maombi yalitishwe na Mchungaji Kiongozi wa Usharika husika na kuwa na viambatanisho vifuatavyo:

1. Cheti cha kuzaliwa.
2. Vyeti vya elimu.
3. Wasifu (CV).
4. Barua ya utambulisho toka serikali ya mtaa.

Zitumwe kwa:

**Afisa Tawala na Utumishi,
KKKT Dayosisi ya Meru,
S.L.P 96, Usa River**

au

kwa barua pepe: hrdme@elctdme.or.tz na info@elctdme.or.tz

Mwisho wa Kupokea maombi ni tarehe 15/12/2021 saa 10.00 jioni

